

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 1055, ARUSHA

Simu : (027) 2503538/ 2507928

Nukushi: (027) 2505973

Barua pepe: rbcarusha@pccb.go.tz

Wavuti : www.pccb.go.tz

ARUSHA-MACHI 30, 2021

TAARIFA KWA UMMA

WAPANDISHWA KIZIMBANI KWA KOSA LA KUOMBA NA KUPOKEA RUSHWA

Ofisi ya TAKUKURU Mkoani Arusha imewafikisha mahakamani Lucas Ng'ida Mollel mkazi wa mtaa wa Kimandolu Arusha na Frank Nicholous Mollel wote wakiwa wafanyakazi wa Kampuni ya uwakala ya Best Support Link Ltd inayokusanya Ushuru wa Maegesho ya Magari katika Jiji la Arusha. Watuhumiwa walikamatwa kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Shilingi elfu Arobaini (Sh. 40,000/-) kutoka kwa Bw. Baihakiyo Shabani ambaye ni Dereva wa daladala na mkazi wa Mlangarini Arusha ili wasimtoze faini ya (Sh. 50,000/-) kwa kosa la kutolipa ushuru wa siku wa daladala.

Awali katika tukio hilo ilielezwa kuwa, mnamo tarehe 26.02.2021 Bw. Baihakiyo akiwa katika shughuli zake za daladala hakuweza kulipa ushuru wa siku wa Shilingi Mia Saba (Sh.700/-) katika kituo cha Kisongo. Baada ya Bw. Baihakiyo kushindwa kulipa usuru huo, mnamo tarehe 27.02.2021 Bw. Lucas, alikamata gari la Baihakiyo lenye namba T. 173 DCK linalofanya safari zake kati ya enewo la Muriet na Moshono Jijini Arusha, na kulihifadhi eneo la Stendi Ndogo Jijini Arusha ambapo alilifunga mnyororo na kumtaka atoe Sh. 40,000/- ndipo aachie gari hilo.

Baihakiyo baada ya kuelezwa hivyo, aliamua kutoa taarifa TAKUKURU Mkoa wa Arusha ambapo mtego wa rushwa uliandaliwa na kufanikiwa kumkamata Bw. Frank Nicolous Mollel akipokea fedha hiyo ya rushwa kwa niaba ya Lucas Ng'ida aliyekuwa amemwelekeza azipokee.

Watuhumiwa walifikishwa katika mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha mnamo tarehe 24.03.2021 na kufunguliwa shtaka ambalo ni CC. Na. 88/2021.

TAKUKURU Mkoani Arusha inawaasa watumishi na wananchi wote wa Mkoa wa Arusha, kuepuka kujihusisha na vitendo vya rushwa, ambavyo vinasababisha kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Imetolewa na:

JAMES G. RUGE – 0738 150 063

MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA